



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

**MAPITIO YA NUSU MWAKA
2019/20**

BENKI KUU YA TANZANIA

Februari 2020



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

**Mapitio ya nusu mwaka
2019/20**

BENKI KUU YA TANZANIA

Februari 2020



Utangulizi

Taarifa hii ya Mapitio ya Nusu Mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha inatoa tathmini ya hali ya uchumi wa nchi na dunia pamoja na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20. Vilevile, taaarifa hii inatoa mwelekeo wa uchumi na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kutekeleza katika kipindi kilichobakia cha mwaka 2019/20.

Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Januari 2020, ukuaji wa uchumi wa dunia ulipungua na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2019, ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 2018. Hali hii ilichangiwa na mgogoro wa kibiashara kati ya China na Marekani, mivutano baina ya mataifa ya Mashariki ya Kati, na changamoto za kisera duniani hususan hatua ya Uingereza kujitoa Jumuiya ya Ulaya. Vilevile, kupungua kwa kasi ya ukuaji uchumi, kulichangiwa na migogoro ya kijamii katika baadhi ya nchi, majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa katika nchi za Karibiani na Australia, na tatizo la ukame katika eneo la kusini mwa Afrika. Hali hiyo, ilichangia kuyumba kwa biashara na uwekezaji. Katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea, ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa mdogo kuliko ilivyotarajiwa mwaka 2019, na kufikia asilimia 3.7, ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2018. Aidha, kasi ya ukuaji uchumi iliongezeka kidogo katika nchi za kusini mwa Jangwa



la Sahara, na kufikia asilimia 3.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2018.

Shirika la Fedha la Kimataifa linakadiriya kuimarika kwa ukuaji wa uchumi wa dunia kwa miaka ijayo. Uchumi wa dunia unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.3 mwaka 2020 na kufikia asilimia 3.4 mwaka 2021 kutokana na kuanza kukua kwa biashara na uwekezaji. Katika nchi zilizoendelea, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 1.6 mwaka 2020 na 2021, wakati ukuaji katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea unakadiriwa kuongezeka na kufikia asilimia 4.4 mwaka 2020 na asilimia 4.6 mwaka 2021. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji unategemewa kuongezeka na kufikia asilimia 3.5 mwaka 2020 na 2021, ikiwa ni matokeo ya kuimarika kwa biashara, na ongezeko la uzalishaji wa mafuta na mazao ya kilimo.

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa mdogo katika nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi pamoja na kuwepo kwa ongezeko kidogo la bei za nishati na chakula. Katika nchi zilizoendelea wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 1.4 mwaka 2019 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 2.0 mwaka uliotangulia. Katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.1 mwaka 2019 kutoka asilimia 4.8 mwaka 2018. Wakati huo huo, mfumuko wa bei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua kidogo na kufikia asilimia 8.4 ukilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2018. Mfumuko wa bei uliongezeka kidogo katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kutokana na ongezeko la bei za vyakula lakini ulipungua katika eneo la nchi za Jumuiya



ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutokana na kupungua kwa bei za vyakula. Kwa mujibu wa taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Januari 2020, mfumuko wa bei unakadiriwa kufikia asilimia 1.7 mwaka 2020 katika nchi zilizoendelea, wakati katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea unakadiriwa kupungua na kufikia asilimia 4.6 kutokana kupungua kwa bei ya nishati. Vilevile, mfumuko wa bei unakadiriwa kupungua katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na kufikia asilimia 8.0 kutokana na matarajio ya kuendelea kupungua kwa bei za mafuta.

Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Tanzania Bara

Uchumi wa Tanzania umeendelea kukua kwa kasi ya juu. Katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2019, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.9 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Ukuaji huu wa uchumi ulichochea zaidi na uwekezaji wa Serikali katika miundombinu, kuimarika kwa shughuli za sekta binafsi, kuimarika kwa mahitaji ya bidhaa na huduma na ukuaji wa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Shughuli zilizochangia sehemu kubwa ya ukuaji huo ni ujenzi, kilimo na usafirishaji. Viashiria vya ukuaji wa uchumi vinaonesha kuwa uchumi katika robo ya nne ya mwaka 2019 umeendelea kuimarika, hivyo basi inakadiriwa kuwa uchumi wa Tanzania utakua kwa asilimia 7 mwaka 2019 na zaidi ya asilimia 7 kwa mwaka 2020.



Mfumuko wa bei umeendelea kuwa mdogo na tulivu katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20. Kwa wastani mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.6 ukilinganishwa na asilimia 3.2 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Kiwango hiki ni chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 na kipo ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (kati ya asilimia 3 hadi 7). Hali hii, ilichangiwa zaidi na utekelezaji mzuri wa sera ya fedha na ya kibajeti, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei usiojumuisa bei za vyakula na nishati ulikuwa ni wa wastani wa asilimia 2.6 ukilinganishwa na asilimia 2.3 kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Mfumuko wa bei unakadiriwa kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20 ikiwa ni matokeo ya uzalishaji wa chakula cha kutosha, kupungua kwa gharama za uzalishaji na utekelezaji mzuri wa sera ya fedha na ya kibajeti.

Ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 9.6 kwa mwaka unaoishia Desemba 2019, na hivyo kukaribiana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 10 ifikapo mwezi Juni 2020. Ukuaji huu, ni matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayoongeza ukwasi katika uchumi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 11.1 kwa mwaka unaoishia Desemba 2019. Ongezeko hilo la mikopo lilielekezwa zaidi kwenye shughuli za kilimo, ujenzi, na madini.



Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20. Hali hii ilitokana na utekelezaji mzuri wa sera ya fedha na ya kibajeti, pamoja na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Utulivu huo wa shilingi ya Tanzania ulichangiwa pia na hatua zilizotekelezwa na Benki Kuu kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri wa ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni nchini.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20, ukusanyaji wa mapato ulivuka malengo ya ukusanyaji kwa mwezi Septemba na Desemba 2019. Mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni TZS 9,810.8 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, sawa na wastani wa makusanyo ya shilingi bilioni 1,635.1 kwa mwezi. Aidha, kiasi hicho ni sawa na asilimia 96.6 ya lengo la makusanyo kwa kipindi hicho. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa sehemu kubwa kulitokana na jitihada kubwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kuhakikisha ulipaji stahiki wa kodi unasimamiwa kwa dhati. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ya Serikali yaliyofanywa kupitia katika akaunti zake zilizoko Benki Kuu, yalifikia shilingi bilioni 10,034.0 ambapo matumizi ya shughuli za maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,639.8. Vilevile, deni la serikali la ndani na nje limeendelea kuwa himilivu. Deni hilo lilikuwa asilimia 27.1 ya Pato la Taifa, chini ya ukomo wa kiwango cha uhimilivu kinachokubalika cha asilimia 70 ya Pato la Taifa. Uhimilivu wa deni unachangiwa na ukuaji endelevu wa uchumi na maboresho ya sera na usimamizi thabiti wa taasisi.



Sekta ya nje imeendelea kuonesha matokeo mazuri ambapo kulikuwa na ziada katika urari wa malipo nje ya nchi na kupungua nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Matokeo haya yalitokana na ongezeko la mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani nje ya nchi. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje inakadiriwa kuwa asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa zaidi ya dola za Marekani bilioni 5.5 mwishoni mwa mwezi Desemba 2019, ambayo inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa zaidi ya miezi 6. Kiasi hicho ni juu ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua 4, ikiwa pia ni juu ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (miezi 4.5) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (miezi 6).

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha zaidi ya kiwango kinachotakiwa kisheria. Kwa ujumla, rasilimali za sekta ya kibenki iliimarika zaidi kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia asilimia 9.8 ya mikopo yote mwezi Desemba 2019 kutoka asilimia 10.7 kwa mwezi Juni 2019. Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya kibenki hasa katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu ili kufikia lengo la asilimia 5. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi za fedha: kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo; utekelezaji wa



mpango kazi wa jinsi ya kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zilizokuwa na uwiano mkubwa; na kutumia kwa lazima taarifa ya historia za wakopaji zilizo kwenye kanzidata ya wakopaji kabla ya utoaji wa mikopo. Aidha, Benki Kuu imezitaka benki za biashara kupeleka taarifa za mikopo kwenye kanzidata hizo, na kutekeleza kanuni za maadili kwa watumishi wa sekta ya kibenki.

Benki Kuu imeendelea kuimarisha udhibiti wa vihatarishi katika sekta ya fedha kupitia utekelezaji wa sera na maboresho ya kanuni mbalimbali za udhibiti. Katika kipindi husika, Benki Kuu ilitoa kanuni za kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha (Financial Consumer Protection Regulations, 2019) mwezi Novemba 2019, na kanuni mpya kwa taasisi ndogo za fedha (Microfinance (Non-Deposit Taking Microfinance Service Providers) Regulations, 2019; Microfinance (Savings and Credit Cooperative Societies), Regulations, 2019; and Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019)) ili kutoa mwongozo wa usimamizi wa taasisi hizo. Kwa upande mwingine, Benki Kuu imeziagiza benki za biashara kutekeleza mpango wa kuimarisha mitaji kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi. Ili kuboresha ufanisi na kuongeza watumiaji wa huduma za fedha, Benki Kuu imeendelea kuchochea ubunifu wa nyenzo mbalimbali za mifumo ya malipo na matumizi ya huduma za kifedha baina ya mitandao ya simu. Katika kipindi husika, mwingiliano wa huduma za kifedha baina



ya mitandao ya simu umechangia kuongezeka kwa miamala ya huduma hizo kwa asilimia 6.0 na ongezeko la thamani ya miamala hiyo kwa asilimia 15.0 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Mpaka mwisho wa mwezi Desemba 2019, idadi ya akaunti zinazofanyakazi na zilizoandikishwa matumizi ya huduma za kifedha baina ya mitandao ilikuwa milioni 24.4 ikilinganishwa na milioni 23.3 mwishoni mwa mwezi Desemba 2018.

Zanzibar

Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2019, ukuaji halisi wa Pato la Taifa la Zanzibar ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 9.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa shughuli zinazotokana na viwanda na biashara. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20 kutokana na uwekezaji wa Serikali kwenye miundombinu ya kijamii (elimu na afya) na miundombinu ya kiuchumi (barabara, viwanja vya ndege na bandari) na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kilimo na utalii.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5. Kwa wastani mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 2.6 ukilinganishwa na asilimia 3.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kilitokana na kupungua kwa bei zisizo za chakula hususan bidhaa za petroli. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya tarakimu moja katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20.



Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, ukusanyaji wa mapato uliongezeka sambamba na usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali. Mapato ya ndani ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 432.0, sawa na asilimia 91.1 ya lengo. Jumla ya matumizi ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 583.9 sawa na asilimia 97.0 ya makadirio, ambapo matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 176.9.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 39.7 katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 33.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Ongezeko la nakisi lilitokana na uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za nje, hususan bidhaa za mafuta na chakula.

Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2019/20

Sera ya fedha ya mwaka 2019/20 imelenga kuhakikisha uchumi unaendelea kuwa na mfumuko mdogo wa bei unaoendana na lengo la muda wa kati la asilimia 5, pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa mwaka unaoishia Juni 2020, sera ya fedha imelenga yafuatayo:

- i. Ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.0;
- ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 13.5 na;
- iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa



na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20 ulikuwa ndani ya malengo yaliyokusudiwa. Uwepo wa mfumuko mdogo wa bei, umeiwezesha Benki Kuu kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi ili kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na hatimaye ukuaji wa uchumi. Katika kipindi husika, Benki Kuu, ilipunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara kutoka asilimia 8 hadi asilimia 7 na kuongeza wigo wa benki kutumia amana hizo kutoka asilimia 10 hadi asilimia 20. Vilevile, Benki Kuu iliongeza ukwasi katika sekta ya kibenki kwa kutumia nyenzo mbalimbali hususan, kwa kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki, na kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la fedha za kigeni.

Utekelezaji wa sera ya fedha umesaidia kuimarika kwa ukwasi katika sekta ya kibenki na kupelekea kupungua kwa riba za masoko ya fedha ya muda mfupi. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.63 mwezi Desemba 2019 kutoka asilimia 5.47 mwezi Juni 2019. Vilevile, riba ya dhamana za muda mfupi ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.81 mwezi Desemba 2019 kutoka asilimia 8.69 mwezi Juni 2019. Wastani wa riba za mikopo ya mabenki kwa ujumla ulipungua hadi asilimia 16.76 mwezi Desemba 2019 kutoka asilimia 16.87 mwezi Juni



2019, na zile za kipindi cha mwaka mmoja zikipungua na kufikia asilimia 16.28 kutoka asilimia 16.43. Vilevile, wastani wa riba za amana kwa ujumla ulikuwa asilimia 6.79 mwezi Desemba 2019 kutoka asilimia 7.44 mwezi Juni 2019, na riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja zilifikia asilimia 8.90 kutoka asilimia 9.06.

Ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi umeendelea kukua kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayoongeza ukwasi katika uchumi. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi umekua kwa wastani wa asilimia 9.6 mwezi Desemba 2019, ukilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10 kwa mwaka unaoishia Juni 2020. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua na kufikia asilimia 11.1 ambapo sekta zilizonufaika zaidi ni kilimo, ujenzi, na uchimbaji wa madini na mawe. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unakadiriwa kuwa asilimia 13.5 kwa mwaka unaoishia Juni 2020.

Katika jitihada za kuendeleza masoko ya fedha ili kuleta ufanisi wa sera ya fedha kuelekea mfumo unaotumia riba, hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwemo kuridhia mfumo wa kisheria wa makubaliano ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi baina ya mabanki (Global Master Repurchase Agreement (GMRA) 2011). Utaratibu huu utaongeza ufanisi na kuhakikisha kuna ukwasi wa kutosha katika masoko ya fedha. Vilevile, Benki Kuu imeendelea kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa soko la fedha baina ya mabanki ili kuchochea mikopo ya muda mfupi na uhamishaji wa dhamana za mikopo.



Mwelekeo wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Pili ya Mwaka 2019/20

Katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayoongeza ukwasi katika uchumi ili kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na shughuli mbalimbali za uchumi sambamba na kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unaendana na lengo la muda wa kati la asilimia 5. Malengo hayo yatafikiwa kutokana na matarajio ya utekelezaji mzuri wa sera ya kibajeti na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuangalia kwa ukaribu kiasi cha ukwasi kwenye mabenki ili kuleta utulivu wa riba katika masoko ya fedha ya muda mfupi. Utulivu wa riba katika masoko ya fedha ya muda mfupi ni hitaji la msingi kuelekea mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba katika kusimamia utulivu wa bei na ukuaji endelevu wa uchumi.

Hitimisho

Uchumi unakadiriwa kuendelea kukua kwa kasi katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20, licha ya changamoto zilizopo za ukuaji mdogo wa uchumi wa dunia. Ukuaji huu unatarajiwa kuchangiwa zaidi na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme, sera thabiti ya fedha na ya kibajeti, usimamizi katika sekta ya madini ikiwamo uanzishwaji wa masoko ya madini, pamoja na matarajio ya hali nzuri ya hewa. Matokeo haya yatasaidia mfumuko wa bei kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20.



Kutokana na makadirio ya kuendelea kwa utulivu wa mfumuko wa bei katika viwango vya chini ya lengo la muda wa kati katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi na kusaidia kukuza shughuli mbalimbali za uchumi. Aidha, Benki Kuu itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi wa ndani na wa dunia kwa lengo la kusimamia utulivu wa mfumuko wa bei kwa kuchukua hatua stahiki katika kutekeleza sera ya fedha. Benki Kuu itaendelea kushirikiana na Serikali katika kusimamia sera ili kudumisha ukuaji endelevu wa uchumi. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau katika sekta ya fedha ili kuhakikisha utekelezaji endelevu wa sera na marekebisho ya kanuni katika kudumisha utulivu wa sekta ya fedha nchini.

Kwa kuzingatia mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa ndani na wa dunia, kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha, utekelezaji thabiti wa sera ya kibajeti, na mwelekeo wa utekelezaji wa sera ya fedha kama ilivyoainishwa katika taarifa hii, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa kwa mwaka wa 2019/20 yatafikiwa.



Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: <http://www.bot.go.tz>